



ukoo :	Yeye ni Muhammad ibn Abdullahi ibn Abdulmuttalib ibn Hashim na Hashim ni kutoka kabila ya qureish na qureish ni katika waarabu na waarabu ni watoto wa
Kuzaliwa:	Alizaliwa katika miaka ya ndovu katika Makkah, mwezi wa Rabbiul awwal, ako na miaka sitini na tatu miongoni wa hizi miaka arobaini kabla ya kupata utume na miaka ishirini na tatu kama nabi na mtume. Alikuwa yatima, babake alikufa kabla ya kuzaliwa kwake, na babu yake Abdulmuttalib ndo alimlea, baada ya kifo cha babu yake alilelewa na mjombake Abu Talib.
Kutumwa :	Alitumwa kwa majini na binadamu, yeyote mwenye daawah yake imemfikia na hajamuamini ni mkafiri mkubwa haijalishi ni nani.
Daawah	Alifanya daawah ya tawheed na akhlaq njema na vitendo na alikataza shirk na akhlaq mbaya na vitendo mbaya.
Israa na	Alipelekwa (Israa) kutoka Makka mpaka Baitul maqdis halafu (Miraj) mpaka mbingu wa saba na akaongea na Allah na akafaradhishiwa salah tano.
Hijra	Alifanya Hijra kutoka Makkah kuelekea Madinah na akafa huko. Na alizikwa katika chumba cha Aisha mama ya waumini,
Kufikish	Allah alimtumia yeye kukamilisha dini na mtume alifikisha vilivyo na alitimiza amanah na aliwapa nasaha ummah na alifanya jihad kwa hakika kwa njia ya
Vita	Ni saba: Badr, Uhud, Khandaq, Kheibar, Fath Makkah, Tabuk, Hunain.
Watoto:	Alqaseem, Ibrahim, Abdullahi (Attayibu Tahir), Zeinab, Ruqaya, Ummu kulthum, Fatima na wote walikufa akiwa hai isipokuwa Fatima alikufa baada yake na miezi sita Allah awarehemu wote
Wakezake:	Khadija, Aisha, Sawda, Hafsa, Zeinab alhilaliya, Ummu salamah hind, Zeinab bint jahsh, Juweiriya bint alharith, Safiya bint huyey, Ummu habibah ramla, Reihana bint zeid, Meimuna bint alharith.
walio	Mama yake Aminah bint wahb, Thuweybah mtumwa wa kike wa mjombake Abi lahab, Halima bint Abi dhuweib saadiyah.
Ayah ya	: ﴿أَفَرَأَى بِأَسْمِ رَبِّكَ الَّذِي خَلَقَ ۱ خَلَقَ الْإِنْسَانَ مِنْ عَلَقٍ ۲ أَفَرَأَى وَرَبُّكَ الْأَكْرَمُ ۳ الَّذِي عَلَّمَ بِالْقَلَمِ ۴ عَلَّمَ الْإِنْسَانَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ۵﴾
Wakwa	Katika wanaume ni Abu bakr Assidique na katika wanawake ni Khadija bint khuweilid mama ya waumini na katika vijana ni Ali ibn Abi Talib na miongoni mwa watumwa walioachwa huru ni Zaid ibn Haritha na miongoni mwa watumwa
Hajj na	Alifanya umrah nne zote katika mwezi wa dhil qaadah na alifanya hajj moja inaitwa hajatul wada' katika miaka ya kumi ya hijra
Tabia yake	Allah amesema Hakika ewe Muhammad uko na tabia tukufu. Aisha mama ya waumini amesema akhlaq ya mtume ilikuwa ni quraan.
Umuhimu ya	Ibn qayyim alisema: kama kufaulu kwa binadamu katika dunia na akhira inalingamana kufuata uongofu ya mtume, basi ni wajib kwa kila anayepatia nasaha nafsi yake na anapenda ifaulu na ifurahi ajue uongofu yake na seerah yake itabawafanya otaka katika watu ambao hawamini yeye na cincia katika idadi ya